

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

CHUO CHA MAJI



Tarehe: 14/12/2020

TAARIFA KWA UMMA

WAZIRI WA MAJI AIAGIZA RUWASA KUSAINI HARAKA MKATABA NA CHUO CHA MAJI ILI KUWATUMIA WAHITIMU WAKE KATIKA MIRADI YA MAJI VIJIJINI

Waziri wa Maji Mh. Jumaa Aweso (Mb) amemuagiza Katibu Mkuu wa Maji, Mhandisi Antony Sanga kumuelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuhakikisha anafika Chuo cha Maji wiki moja kuanzia leo tarehe **14.12.2020** kusaini makubaliano ya jinsi ya kuwatumia wahitimu wa Chuo cha Maji kuisimamia na kuiendesha miradi yote ya maji vijijini iliyokwisha kamilika.

Mheshimiwa Waziri ametoa maagizo hayo alipokuwa kwenye ziara yake katika Chuo cha Maji ambapo alikutana na Bodi ya Ushauri ya Chuo hiko, Watumishi pamoja na Wanafunzi. Wakati akitoa agizo hilo alisisitiza kuwa, Wizara ya Maji na Serikali kwa ujumla inaingia gharama kubwa katika kukiendesha Chuo hiki lakini wataalamu wenye weledi mzuri wanaozalishwa hawatumiki ipasavyo kuleta tija ndani ya Sekta ya Maji Nchini.

Mh. Jumaa Aweso (Mb) alisema “*haiwezekani miradi ya gharama kubwa inayojengwa na Wizara ikapoteza ubora mapema sababu ya kukosa usimamizi wa Wataalam, wakati Chuo chetu kinazalisha kwa juhudi vijana wengi ambao ni nguvu kazi ya Taifa, nakuagiza Katibu Mkuu umwambie Mkurugenzi wa RUWASA afike haraka Chuoni hapa, wasaini makubaliano na vijana waanze kazi mara moja kwani fedha za kuendesha miradi zipo.*”

Aidha, watumishi wa Chuo Cha Maji pia walikumbushwa kuendelea kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu kwa wanafunzi wao kwani Sekta ya Maji inawategemea sana wahitimu wa Chuo hiki katika kutimiza lengo la serikali la kufikisha huduma ya Maji kwa kila Mtanzania.

Mwisho, Waziri alimaliza ziara yake Chuoni hapo kwa kutembelea nyumba mbili za Taasisi ambazo ziliuzwa nje ya utaratibu na kumuagiza Mkuu wa Chuo Dkt. Adam Karia na Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo Prof. Felix Mtalo kuhakikisha taratibu za kurejesha nyumba hizo chini ya umiliki wa Serikali unafanyika kwa haraka sana. Na alipongeza juhudi za makusudi ambazo Chuo cha Maji kinazifanya katika kutoa mafunzo bora na kutimiza wajibu wa kuanzishwa kwake.



Ghanima Chanzi

Mkuu Kitengo cha Mawasiliano

Chuo cha Maji